Emergency
Medical Services

**Ref. EPLUS/PHAB/REG/01/22** **13th January 2022**

The Executive Director,
Tanzania Investment Centre,
Plot No. 9 A & B, Shaban Robert Street,
P. O. Box 938
DAR ES SALAAM

Dear Sir,

**RE : COVERING LETTER FOR APPLICATION FOR CERTIFICATE OF INCENTIVES WTH THE TANZANIA INVESTMENT CENTRE,**

Reference is made to the heading above.

We are pleased to present our application with your esteemed Centre for a grant of a certificate of incentives. Please find enclosed list of documents as part of the requirements for the said application:

(i) A copy of our project's Business Plan

(ii) A dully filled in TIC application form

(iii) A copy of the company's Memorandum and Articles of Association.

(iv) A certified copy of the Certificate of Incorporation.

(v) Proof of funds related to the project

(vi) Certified copy of our lease agreement over the project location

(vii) Board Resolution approving the company to register the project with the TIC

The contact persons in respect of this application shall be:

Emergency Medical Services

1. Mr. Amir Mwamba +255 784 360000
2. Dr. Deodatus Mtasiwa +255 754 474346

Yours Faithfully,

**EMERGENCY PLUS MEDICAL SERVICES TANZANIA LIMITED**

**ABBAS GEDI GULLET**
**CHAIRMAN**

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

BARUA ZOTE ZITUMWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA

**Tel:** 2170173
2171022
**Fax:** 2172606

**Unapojibu tafadhali taja :**
**Kumb. Na. KMC/HEALTH/A.1.7/61**

**OFISI YA MGANGA MKUU**
**MANISPAA YA KINONDONI**
**S. L. P. 61665,**
**DAR ES SALAAM**

**Tarehe 31 DESEMBA, 2021**

**TAARIFA YA UKAGUZI WA JENGO LA EMMERGENCY PLUS MEDICAL SERVICES TANZANIA LTD MIKOCHENI MANISPAA YA KINONDONI DAR ES SALAAM.**

## UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ina wajibu wa kusimamia huduma za afya zilizo bora na salama kwa wananchi wote wa Manispaa hii, ili kutekeleza wajibu huo, Manispaa inapaswa kuhakikisha sera, kanuni na miongozo yote iliyotolewa inafuatwa na vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Madhumuni ya ukaguzi huo ni kwenda kufanya tathmini katika maeneo kama yanafaa kutolea huduma za afya kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo ya utoaji wa huduma za afya nchini.

## A)MALENGO YA UKAGUZI

i. Kukagua jengo kwa macho,uimara na kushauli jinsi mpangilio wa vyumba vitakavyokuwa. (Flow pattern)
ii. Kukagua na kuangalia mazingira ambayo kituo kinapojengwa kama yapo salama kwa afya za wanainchi.
iii. Kukagua na kuangalia kiwango na ubora wa maji yanayotumika.
iv. Kukagua na kuangalia kama umeme wa TANESCO upo, ikiwa na pamoja na Generator la dharula.
v. Kukagua na kuangalia mazingira ya jengo kwa ujumla (usafi)
vi. Kukagua na kuangalia kama kuna muingiliano na nyumba za kuishi.

## LENGO MAHUSUSI

**Lengo la ukaguzi huu lilikuwa ni kukagua jengo/eneo la kutolea huduma za Dharula (Emmergency - Ambulance services) jengo lililokaguliwa ni nyumba namba 18 mtaa wa Chato – Regent estate.**

## JINSI UKAGUZI ULIVYOFANYIKA

(i) Wajumbe kujitambulisha kwa mmiliki/msimamizi wa kituo na kuwaeleza madhumuni na matarajio ya ukaguzi katika kituo hiko.

(ii) Timu iliyoongozana na mmiliki/msimamizi wa kituo kukagua jengo na maeneo muhimu.

(iii) Kutoa mrejesho wa ukaguzi kwa mmiliki/msimamizi wa kituo na kujadiliana kuhusiana na changamoto katika kutoa huduma hii ya afya.

(iv) Kuweka agano na mmiliki/msimamizi wa kituo jinsi ya kutekeleza mapungufu yatakayojitokeza.

(v) Kuandaa ripoti ya ukaguzi kuwasilisha kwa Mganga Mkuu wa Manispaa na kwa mmiliki.

## B) MAMBO MAZURI YALIYOJITOKEZA

I. Jengo lipo kwenye mazingira mazuri ambapo maeneo hakuna Supermarket, Malls, bar au Gas Filling Station.

II. Kituo kina sehemu kubwa ya kutosha kuweka viti vya kutolea huduma.

III. Kituo kina sehemu ya kuegesha magari ya wasindikizaji wagonjwa.

IV. Kuna mwanga na hewa ya kutosha.

V. Mfumo wa umeme wanatumia Grid ya Taifa.

VI. Mfumo wa maji safi na maji taka mzuri wanatumia maji ya Dawasco.

VII. Kuna matank kwa ajili ya kuifadhia maji ya akiba

VIII. Kituo wana vyoo vya kutosha pamoja na wenye uhitaji maalumu.

IX. Kituo kimejenga kwa vifaa vya kudumu.

## C) CHANGAMOTO

Kuongeza vyoo vya nje pamoja na cha watu wenye huitaji maalumu

Kukata partion kwa ajili ya mapokezi.

Kuweka fenicha katika kila chumba husika

## D) HITIMISHO

Timu imeridhika na namna ambavyo mmiliki wa kituo amejipanga kutoa huduma ya **DHARULA (EMERGENCY)** katika eneo hilo. Kituo ni kizuri sana cha msingi ni kufuata ushauri na kuzingatia mwongozo, kanuni, sheria na taratibu zilizowekwa na Wizara inayosimamia utoaji wa huduma za afya nchini.

## E) TIMU YA WAKAGUZI

- Dr. Nassoro Mwagara Private Cordinator Manispaa ya Kinondoni
- ANGASYEGE KAFUKO LB/CO
- EXAVERY MWAULAMBO H/O
- Dr. PAULO MAPILI RAD/CO
- DR EMMANUEL KOMBE EMERGENCY CO

Kny:MGANGA MKUU WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI